
# Habari za TASAF

# ARUSHA DC

TOLEO MAALUM, 2022



Mradi wa Mabweni mawili ya wavulana katika shule ya Sekondari Oldonyowas uliotekelezwa kwa gharama ya shilingi milioni 300 ukiwa na uwezo wa kubeba wanafunzi 160.




# HABARI ZA TASAF

## HALMASHAURI YA ARUSHA

Serikali kupitia Mfuko wa Maendelo ya Jamii (TASAF) inatekeleza Miradi mbalimbali kisekta Nchini kwa lengo la kusaidia kupunguza kiwango cha umasikini kwa kuboresha maisha ya kaya ili kuizinua kiuchumi.

Halmashauri ya Arusha ni miongoni mwa Halmashauri Nchini inayonufaika na Miradi ya TASAf ikiwemo Mradi wa uhawilishaji fedha kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini, kuboresha miundombinu katika Sekta ya Elimu, Afya, ajira za muda na uwekaji wa akiba kwa vikundi vya walengwa.

Katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 ya Julai - Septemba 2022, Halmashauri ilipokea kiasi cha shilingi Bilioni 1.4 za TASAF, shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya uhawilishaji fedha kwa walengwa 14,612 na shilingi Milioni 300 zikitumika katika ujenzi wa bweni la wavulana shule ya sekondari Oldonyowas.

Mwenyekiti Halmashauri ya Arusha, Mhe. Ojung'u Salekwa kwa niaba ya wananchi na uongozi wa Halmashauri, wanaishukuru na kuipongeza Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kupitia TASAF kwa kutekeleza miradi inayolenga moja kwa moja kukwamua maisha ya wananchi wasio na uwezo kutoka kwenye lindi la umasikini uliokithiri.

## YALIYOMO

Uboreshaji wa Miundombinu........................................1

Miradi ya Ajira za muda........................................3

Miradi ya Kukuza Kipato cha Kaya........................................5

Vikundi vya Kuweka na Kukopa........................................6

Uhawilishaji wa Fedha kwa Walengwa........................................7

Mafunzo kwa Walengwa wa TASAF........................................9



# BAADA YA BWENI LA WASICHANA, TASAF YAWAKUMBUKA WAVULANA SHULE YA SEKONDARI OLDONYOWAS

**Na Elinipa Lupembe**

Katika kutekeleza mkakati wa kuboresha miundombinu ya shule, serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii -TASAF, imewakumbuka wavulana wa shule ya sekondari Oldonyowas, kwa kutoa fedha kwa ijali ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mabweni mawili ya wavulana shule ya sekondari Oldonywas, halmashauri ya Arusha, baada ya kujenga mabweni mawili ya wasichana shuleni hapo.

Akizungumza wakati wa kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo, mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, ameweka wazi kuwa, kwa mara nyingine tena, serikali kupitia mfuko wa TASAF imetoa fedha, kiasi cha shilingi milioni 320, kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili ya kulala wanafunzi wavulana 160, shule ya sekondari Oldonyowas, hii ni baada ya awamu ya kwanza kujenga mabweni mengine mawili ya wasichana kwa shule hiyo.

Mkurugenzi Msumi amethibitisha umuhimu wa shule hiyo kuwa na mabweni kwa wanafunzi wa jinsi zote, ni kutokana na asili ya mazingira ya eneo hilo, watoto wengi wanaishi mbali na shule na kusababisha kitembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni, jambo ambalo linawaathiri kiafya, kisaikolojia na hata kitaaluma.

"Ninampongeza Rais wetu, Mama Samia kwa kusikia kilio cha watoto wake, watoto wa Oldonyowas, na kujenga mabweni ya wavulana pia, tunaamini uwepo wa mabweni utaongeza ari ya wanafunzi kupenda shule, kutapunguza watoto kuacha shule, kwa kuwa na mazingira tulivu ya kujisomea, jambo ambalo litapandisha taaluma shuleni na kuongeza kiwango ya ufaulu kwa wanafunzi " Amefafanua Mkurugenzi Msumi

Naye Michael Ismail mwanafunzi wa kidato cha nne, licha ya kuishukuru serikali ya awamu ya sita, amefurahishwa na kitendo cha kujengwa mabweni ya wavulana shuleni hapo, ambapo awali kulikuwa na mabweni ya wasichana peke yao na kuongeza kuwa wanafunzi wengi hukosa muda wa kujisomea wawapo nyumbani, kutokana na uchovu wa kutembea umbali mrefu, huku wazazi wakiwapangia majukumu ya kazi za nyumbani mara watokapo shuleni.

"Watoto wengi wanaishi mbali na shule lakini wakifika nyumba watapewa kazi za kuchunga ama kukata majani ya mifungo, jambo ambalo linatukosesha muda wa kujisomea hasa tuwapo nyumbani, lakini tukiwa na mabweni itatusaidia kutumia muda mwingi kujisomea kwa pamoja na kuturahisishia kufanya kazi za shule kwa kujadiliana katika makundi 'group discussion'". amefafanua mwanafunzi Michael

Mradi huo wa ujenzi wa mabweni mawili ya wavulana shule ya sekondari Oldonyowas, unafanya kuwa na idadi ya miradi tisa tofauti iliyotekelezwa na TASAF katika shule hiyo, ikiwemo vyumba vya madarasa, mabweni mawili ya wasichana, jengo la utawala, matundu ya vyoo, nyumba za walimu.



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Deogratius John Ndejembi, akikagua mradi wa ujenzi wa Mabweni ya wavulana shule ya sekondari Oldonyowas, mradi unaotekelzwa na TASAF kwa gharama ya shilingi milioni 300*

# NAIBU WAZIRI NDEJEMBI AIAGIZA TASAF KUTEKELEZA UJENZI WA UZIO SHULE YA SEKONDARI OLDONYOWAS

**Na Elinipa Lupembe**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Deogratius John Ndejembi ameuagiza uongozi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kutekeleza ujenzi wa uzio katika shule ya sekondari Oldonyowas ili kulinda Miundombinu ya madarasa na mabweni iliyojengwa katika shule, ikiwa ni pamoja na usalama wa wanafunzi wa shule hiyo.

Naibu Waziri Ndejembi amesema hayo wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa ujenzi wa mabweni mawili ya wavulana katika shule hiyo, Mradi unaotekelezwa na TASAF III awamu ya II kwa ufadhili wa OPEC International Fund, na kuweka wazi kuwa, kukamilika kwa miundombinu ya shule hiyo, uende sambamba na ujenzi wa uzio wa shule hiyo ili kuhakikisha usalama wa shule na wanafaunzi.

"Nimeridhishwa na maendeleo ya ujenzi huu wa mabweni kutokana na ushirikishwaji wa wananchi wa eneo hili, kwa kuwapa ajira za muda na kujipatia kipato kama ilivyo mpango wa TASAF wa kuzikomboa kaya zenye kipato cha chini, niwatake TASAF kuweka mkakati wa kujenga uzio katika shule hii kwa ajili ya usalama wa mali na wanafunzi". Amesema Mhe. Ndejembi

Naye Mbunge wa jimbo la Arumeru Magharibi Mhe. Noah Lembris amesema kuwa uwepo wa mabweni hayo utasaidia utulivu kwa wanafunzi hasa wale wanaotembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni kuondokana na adha hiyo, hali itakayochangia kupanda kwa taaluma na ongezeko la ufaulu kwa wanafunzi shuleni hapo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhandisi Richard Ruyango, licha ya kuishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni hayo, amewataka viongozi pamoja na wananchi kila mtu kutekeleza wajibu wake kama kanuni na taratibu za serikali zinavyoelekeza ikiwemo kutunza na kulinda miradi yote inayotekelezwa na Serikali katika maeneo yao.

Awali akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Oscar Maduhu, amesema kuwa lengo la miradi hiyo ni kuondoa adha iliyopo katika maeneo yenye uhaba wa miundombinu katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya elimu na afya, lengo likiwa ni kupambana na adui maradhi, ujinga na umasikini.

"TASAF itaendelea kutekeleza miradi mingine kwa ajili ya kuwahudumia wananchi kisekta, niwatake wananchi kuendelea kujitoa katika kutekeleza miradi pamoja na kuhakikisha miradi hiyo, inakamilika kwa viwango vinavyokubalika, ili kufikia lengo la serikali la kuwahudumia wananchi wa kipato cha chini, zaidi niwatake kuitunza miradi hiyo ili idumu kwa muda mrefu na kuhudumia wanafunzi wetu". Amesisitiza Maduhu.

Elieshi Gabriel ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Oldonyowas ameweka wazi kuwa, Watoto wao walikuwa wanatembea umbali mrefu sana wakivuka makorongo makubwa kufika shuleni hapo, na wakifika nyumbani wanakuwa wamechoka sana kiasi cha kutoweza kujisomea wenyewe hivyo uwepo wa mabweni hayo utasadia Watoto wao kuwa salama na ufaulu wao kuongezeka.

Mradi huo wa ujenzi wa mbweni mawili ya wavulana umetekelezwa kwa gharama ya Zaidi ya shilingi milioni 300 baada ya kukamilika kwa mabweni ya wasichana katika shule hiyo na yanatarajiwa kubeba jumla ya wanafunzi 160.



# TASAF YAWEZESHA UJENZI WA KIVUKO MOIVO, HUKU KAYA ZILIZO KWENYE MPANGO ZIKINUFAIKA NA AJIRA ZA MUDA

**Na Elinipa Lupembe**

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF kupitia mradi wa mpango wa kunusuru kaya Masikini, unaendelea kuzinufaisha kaya hizo, kwa kutoa ajira za muda kupitia miradi iliyoibiliwa na kaya hizo na kutekelezwa katika maeneo yao.

Kijiji cha Moivo, kata ya Moivo ni miongoni mwa vijiji 88 vya halmasahauri ya Arusha, vinavyonufaika na mpango huo unaotekelezwa na TASAF awamu ya III, kikiwa na walengwa 250.

Akizungumza kwenye eneo la ujenzi wa kivuko hicho, mwenyekiti wa kamati ya Ujenzi Brazard Mkwizu, amesema kuwa mradi wa ujenzi wa kivuko uliibuliwa na walengwa hao, kutokana na adha kubwa waliyokuwa wakiipata wananchi wa eneo hilo kwa kukosekana kivuko, na kuwasilishwa halmashauri, hatimaye TASAF.

Mkwizu ameweka wazi kuwa eneo hilo lilikiwa ni eneo hatarishi kwa wananchi wa Moivo, nyakati zote za mwaka, huku wahalifu wakitumia eneo hilo kukaba na kunyang'anya watu mali zai, wengine kubakwa huku wengine wakinusurika kuuwawa.

Hata hivyo wanufaika hao wamethibitisha kuwa licha ya TASAF kutatua changamoto ya kivuko katika eneo lao, lakini walengwa hao wamekuwa wakifanya kazi za muda na kulipwa ujira, pesa ambayo huwasaidia kujikimu kimaisha.

"Tunaishukuru serikali kwa kutujengea kivuko, kwa kuwa eneo hili lilikiwa ni hatari hasa nyakati za usiku na alfajiri, vibaka waligeuza kichaka cha wanyang'anyi, tunategemea tatizo hili litakwisha, lakini zaidi sisi walengwa tumepata ajira za muda licha ya kuwa pesa si nyingi sana ila sio sawa na kukosa kabisa, tunafanya kazi kwa moyo kwa kuwa kivuko hiki, kitatusaidia wakazi wote wa Moivo". Amesema Tatu Hamisi mnufaika wa mpango wa Kunusuru kaya Masikini

Naye mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, amewataka wananchi hao kujitoa kwa moyo wakati wote wa ujenzi mpaka kukamilika kwa kivuko hicho, na akiwasisitiza kukitunza mara baada ya kukamilika.

"Mnapaswa kutambua namna serikali inawathamini na kutatua kero iliyokuwa inawkabili, rai yangu ni kutunza miundo mbinu ya kivuko hiki kwa kiwa serikali intumia fedha nyingi katika kutekeleza miradi, wananchi mnapaswa kuithamini miradi yote" amesisitiza Msumi.

Awali TASAF imetoa kiasi cha shilingi milioni 76 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kivuko, huku shilingi milioni 38 zikitumika katika ujenzi na milioni 38 zikitumika kulipa ujira kwa wanakaya walio kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini katika kijiji hicho cha Moivo, kwa kufanya kazi za muda kwa masaa na kwa zamu kila siku.



# TASAF YAONDOA CHANGAMOTO YA KIVUKO KITONGOJI CHA MOIVO.

**Na Elinipa Lupembe**

Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF imetekeleza mradi wa ujenzi wa kivuko kitongoji cha Moivo kata ya Moivo halmashauri ya Arusha, changamoto ambayo ilihatarisha maisha ya watu na mali zao wa eneo hilo.

Wakizungumza mara baada ya Mkurugenzi Mtendaji halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, kuzindua Kivuko hicho, wananchi wa Moivo licha ya kuishukuru TASAF kwa kuwajengea kivuko, wameeleza madhara yaliyowapata kabla ya kuwa na kivuko ni pamoja na watu kuporwa mali zao na vibaka, wanawake kubakwa huku wengine wakinusurika kuuawa na watoto kushindwa kwenda shule hasa wakati wa mvua kwa kushindwa kupita hapo.

Eliamani Shange ambaye ni mnufaika wa TASAF, ameweka wazi kuwa, kuwepo kwa kivuko hicho sasa kumeondoa kero zote hizo, hakuna tena kichaka cha vibaka hapo na kubwa zaidi sasa watoto wanakwenda shule kwa amani, huku kivuko hicho kikitarajiwa kukuza uchumi wa eneo hilo kwa kuwa wafanya biashara wanasafirisha bidhaa zao kwa urahisi tofauti na hapo mwanzo.

"Hiki kivuko kimetusaidia sana kina mama na watoto, lakini pia kimewarahisishia wajasiriamali kusafirisha bidhaa zao, kama unavyoona magari sasa yanapita hapa yamebeba bidhaa mbalimbali, zamani watu tulibeba kichwani, tunaishukuru sana TASAF ni mkombozi wa jamii na mali zao, usafiri ni wa uhakika usiku na mchana" amesisitiza Mwajabu Hassan

Naye Diwani wa kata ya Moivo Mhe. Selina Mollel, ameipongeza serikali kupitia TASAF kwa kuwaondolea wananchi wake kero ya muda mrefu, sambamba na kuwapongeza walengwa wa TASAF kwa kujenga kivuko hicho kwa mikono yao kupitia mpango wa ajira za muda unaowawezesha walengwa kufanya kazi katika miradi hiyo

"Kipekee niwapongeze walengwa wa TASAF, mmefanya kazi kubwa na nzuri, mmesimama imara na kuhakikisha kivuko kimepatikana kama lilivyokuwa hitaji lenu la muda mrefu, mmefanya kazi kwa moyo bila kukata tamaa, hadi ujenzi umekamilika, serikali yetu inahitaji wananchi wazalendo kama ninyi" Amesisitiza Mhe. Selina.

Hata hivyo Mkurugenzi Mtendaji, halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, amewataka wananchi hao wa Moivo, kukitunza kivuko hicho ili kidumu na kuwaletea mabadiliko ya kijamii na kiuchumi, kwa kuwa tayari serikali imetimiza jukumu lake la kuwawekea miundombinu hiyo kazi yao ni kutumia na kutunza na kusisitiza kuwa mama Samia ameupiga mwingi.

"Kuwepo kwa kivuko katika eneo hili, ni chanzo cha maendeleo katikaneneo hili, kitarahisisha kusafirisha mazao, kuasafirisha bidhaa kwa wafanayabiashara na hata suala la wagonjwa litakuwa rahisi, ambulance zitafika sasa hadi nyumbani" amesisitiza Msuimi

Awali mradi wa Kivuko cha Moivo, umetekelezwa na TASAF kupitia programu za ujenzi wa miundombinu na Ajira za muda, kwa gharama ya shilingi milioni 68 huku asilimia 50 ya fedha hizo zikitumika kununua vifaa na asilimia 50 ikitumika kulipa ujira kwa wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya masikini kwa lengo la kuwaongezea kipato.



*Janeth John, mlengwa na mwenyekiti wa kikundi cha UPENDO - TASAF akiwa kwenye genge lake la mbogamboga, biahsara ambayo mtaji wake ameupata kutokana na kikundi cha kuweka na kuwekeza.*

# VIKUNDI VYA WALENGWA WA TASAF VYAINUA UCHUMI WA KAYA

**Na Elinipa Lupembe**

Wanufaika wa mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, mradi unaotekelezwa Serikali kupitia Mfuko wa Maendelo ya Jamii - TASAF III awamu ya pili, wameanza kunufaika kiuchumi kupitia vikundi vya kuweka na kuwekeza, vikundi vilivyoviunda na walengwa hao, halmashauri ya Arusha.

Walengwa hao wa kijiji cha Oltulelei kata ya Ilboru, wameweza kuinua vipato vya familia zao kwa kujipatia mitaji ya kuanzisha miradi midogo midogo, kupitia programu ya vikundi vya TASAF vya kuweka, kuwekeza na kukopa.Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye maeneo ya biashara zao, wana kaya hao wamethibitisha kuwa, licha ya kupokea fedha za ruzuku ya mwezi, lakini pia walijengewa uwezo wa kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa kupitia fedha za ruzuku wanazopokea.

Janeth John mlengwa na mwenyekiti wa kikundi cha UPENDO -TASAF anayemiliki genge la kuuza mbogamboaga kwa sasa, amesema kuwa watalamu waliwajengea uwezo wa kuanzisha vikundi vya kuwekeza pesa kutokana na ruzuku wanayoipa kutoka TASAF,na bada ya kuanzisha kikundi kimewawezesha kupata mitaji na kuongeza kuwa kila mwanakukundi ameshaanzisha biashara yake sasa Kikundi chetu kina wana wanachama 10, tulianza tukiwa na hofu sana, lakini kikundi kimetuwezesha kupata mitaji ya kuanzisha biashara, biashara ambazo zimepunguza ugumu wa maisha, biashara zimewawezesha wanakikundi hao kuwekeza, kukopa na kurejesha kwa wakati, na kuongeza kuwa, walipoanza kikundi wengi wao hawakuwa na biashara, na kwa sasa wanachama wote wana biashara, biashara ambazo zimewawezesha kujimudu kimaisha kwa kila mmoja mwanakikundi.

"Hapo mwanzo hatukuamini kama jambo hili kama litawezekana, kutoka na kiasi cha oesa tunachopokea, lakini tumeweza kugonga hisa kila wiki, tuna mfuko wa jamii ambao tunasaidiana kutatua changamoto za kijamii kama msiba na ugonjwa, lakini zaidi tumeweza kukopeshana na kupata mitaji, inayotuwezehsa kuendelea kuweka akiba, kukopa na kupata marejesho, huku faida ya biashara ikituwezesha kuhudumia famialia zetu " amesisitiza Janeth.

Rabisante Mwanga, mwanakikundi cha UPENDO na mama wa watoto watatu, amebainisha kuwa, kupitia kikundi chao cha UPENDO TASAF, ameweza kupata mtaji wa shilingi 150,000 wa kuuza mitumba, mradi ambao unampatia kipato cha kumudu maisha yake na familia yake huku akiwa na matarajio ya kukuza mtaji na kuanza kununua mitumba kwa jumla maarufu kama 'belo'.

Dina Yoram, mlengwa anayemiliki genge na sehemu ya kuchoma samaki na mihogo, amefafanua kuwa, Kikundi chao kimewawezesha kuongeza kipato cha familia yake, na kumfanya kumudu mahitaji ya muhimu kwa familia yake na kuwataka wanawake waaibweteke badala yake kutumia futsa hizo za vikundi kuanzisha biashara ili kupambana na hali ya umaaikini.

Hata hivyo Dina Emson, amewaka wazi kuwa kabla ya kuanza kupokea pesa za TASAF alikuwa na ujuzi wa kusuka, akisuka wateja wake eneo lisilo rasmi, baada ya kujiunga na kikundi cha TASAF amefanikiwa kufungua saloon, eneo ambalo limemuwezesha kupata wateja zaidi, mtaji ambao unamudu kulipa kodi ya pango pamoja na kuhudumia familia yake.

"Nilikuwa na ujuzi wa kusuka nawafuata wateja nyumbani, jambo ambalo lilinigharimu nauli ya kwenda na kurudi, kwa sasa wateja wangu wananifuata hapa hapa saloon kwangu, kadri siku zinavyokwenda natarajia kuweka vifaa vyote vya saloon na saloon yangu iwe kubwa zaidi"amesistiza Upendo.

Mpango wa Kunusuru kaya masikini, wenye lengo la kukuza pato la familia, umekuwa na programu ya vikundi vya kuweka na kuwekeza kwa walengwa walio kwenye mpango ili kukuza uchumi wa kaya program ambayo imeanza kuzaa matunda kwa baadhi ya Kaya hizo.

# TASAF YAWEZESHA KAYA KUANZISHA VIKUNDI VYA KUWEKA NA KUKOPA

**Na Elinipa Lupembe**

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF, kupitia Mpango wa Kunusuru kaya Masikini, umekuwa na programu ya wanufaika wa mpango kuunda vikundi vya kuweka, kuwekeza na kukopa lengo likiwa ni kuwajengea uwezo wa kujiinua kiuchumi kupitia vikundi hivyo.

Kama ilivyo kawaida ya vikundi vingine vya kuweka na kukopa, wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya masikini kijiji cha Mungushi kata ya Bwawani, wamefanikiwa kuwa na kikundi imara kilichoanza miaka mitatu iliyopita.

Mwandishi wa habari hizi alifanikiwa kukutana na wanakikundi hao, siku ya malipo ya ruzuku ya mwezi 7/8, na kuzungumza na wanufaika hao, ambao wameweka bayana kuwa, walianzisha kikundi chenye jumla ya wanakikundi 15 na kukipa jina la CHIPUKIZI GROUP, kikundi ambacho kimewawezesha kuongeza kipato cha kaya, kinachowawezesha kumudu kupata mahitaji muhimu ya kaya zao.

Katibu wa kikundi cha CHIPUKIZI, Grace Sayale, amesema kuwa walipata mafunzo ya uundaji wa vikundi vya kuweka, kuwekeza na kukopa kutoka kwa wawezeshaji wa TASAF, na kuamua kujiunga kwenye kikundi na kuanza kuweka fedha na kukopeshana kwa riba ya asilimia 5 na hukutana kila wakati wa malipo ya ruzuku ya TASAF.

Aidha Grace ameishukuru Serikali kupitia TASAF kwa kuwawezesha kifedha, kwa kuwa hapo awali maisha yalikuwa magumu kwao na familia zao, kwa sasa kina mama wengi wameamka kiakili na kifkra, kila mwanamke anapambana kuwa na shughuli inakayomuingizia kipato tofauti na zamani.

"Kikundi kimetusaidia kukutana na kubadilishana mawazo ya kimaendeleo, wamama wengi wameamka na hata wasio walengwa wa TASAF, wanafanya kazi za kuingiza kipato, hakuna mwanamke siku hizi ana muda wa kupiga umbeya, zaidi tunajivunia kuwa na Rais mwanamke naye ametufanya tujiamini zaidi" Amefafanua Grace

Naye Mweka Hazina wa Kikundi cha CHIPUKIZI, Paulina Thomas, amefafanua kuwa, wao kama wanakikundi wana malengo ya kufika mbali kiuchumi, hivyo wanatumia pesa za ruzuku wanazipata kupitia TASAF kuweka na kukopa na kufanyia miradi midogomidogo ya ujasiriamali, kilimo na ufugaji.

"Tumewekeana mikakati kabla ya kumkopesha mwanakikundi, tunahakikisha ana malengo na kutuchanganulia matumizi ya fedha hiyo na mipango ya urejeshaji, ili mtu asikope pesa bila malengo" Amefafanua Mweka Hazina Paulina

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini, unaendelea kutekeza miradi mbalimbali, lengo likiwa ni kwejengea uwezo wanakaya wa kujikimu kimaisha, unaokwenda sambamba na maendeleo ya kijamii katika sekta za afya, elimi na uchumi wa kaya.



*Wanakikundi cha Chipukizi Group' wakiwa kwenye shughuli za kikundi za kukusanya pesa ya wekeza kwenye ofisi ya kikiji cha Mungushi mara baada ya kupokea ruzuku ya fedha za TASAF kwa mwezi 7/8 2022*



Afisa Mtendaji wa kijiji cha Laroi, Saning'o Moiyo, (aliyeshikamkaratasi) akisoma majina ya wanakaya mpango wa Kunusuru kaya masikini waliofika kupokea ruzuku ya malipo ya mwezi 7/0 2022, kwenye ofisi ya kijiji hicho

# WALENGWA TASAF WATAKIWA KUTIMIZA MASHARTI YA RUZUKU YA FEDHA

**Na Elinipa Lupembe**

Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, mradi unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF awamu ya IV, wametakiwa kutimiza masharti ya msingi ya ruzuku ya fedha wanazozipokea ili kuimarisha sifa za kuwa kwenye mpango.

Akizungumza wakati wa zoezi la ugawaji ruzuku ya fefha kwa mwezi wa 7/8, 2022, Mratibu wa TASAF halmashauri ya Arusha, Grace Makema, amesema kuwa, TASAF inatoa fedha hizo kwa walengwa zikiwa na masharti ya kutimiza, ili mlengwa aendelee kuwa na sifa za kupokea ruzuku hiyo.

Amewataka walengwa hao kuzingatia masharti hayo, ikiwa ni pamoja na masharti ya afya kwa kaya zenye watoto wa kuanzia miaka 0-5, kwa kuhakikisha watoto hao, wanahudhuria kliniki kwa kipindi chote, pamoja na kupata chanjo zote stahiki kwa miaka hiyo mitano.

Ameongeza kuwa, kaya pia zinatakiwa kuzingatia masharti ya elimu, kwa kaya zenye watoto wa miaka 6-18, kuhakikisha wanakwenda shule na kuhudhuria masomo ya kwa siku zote bila kukosa huku wakiwapatia watoto hao mahitaji muhimu ya shule.

"TASAF imeandaa utaratibu wa kufanya Warsha za Jamii, ili kutoa mafunzo kwa walegwa kila wakati wa zoezi la kugawa ruzuku, hivyo tunasisitiza kila mlengwa kuhudhuria warsha za jamii, ili kuendelea kupata ufahamu zaidi wa huduma zinazotolewa na mpango, haki, wajibu na umuhimu wa kutimiza masharti ya ruzuku" . Amefafanua Mratibu Grace.

Hata hivyo walengwa wa kijiji cha Laroi, wamepongeza, serikali kupitia TASAF kwa kuziwezesha kaya zao kiuchumi, huku wakiendelea kupewa elimu ya matumizi ya fedha na kutambua haki na wajibu wao kama wanufaika wa mpango huo, Mwenyekiti wa kijiji cha Laroi, Mhe. Remingi Joseph, amebainisha kuwa uwepo wa program mbalimbali za mafunzo kwa walengwa unasaidia walengwa na jamii kupata uelewa wa pamoja juu ya miradi ya TASAF na ruzuku za fedha wanazopokea walengwa.

"Mradi wa TASAF licha ya kuwainua kiuchumim lakini pia umewafanya wananchi kuchangamsha akili na kubadilika kifikra kwa kuwa wanajumuika na wenzao kwenye vikundi na miradi lakini zaidi wanapata mafunzo yanayowawezesha kubadilika na kukua kifikra" Ameweka wazi mhe. Remigi

Awali katika dirisha la mwezi wa 7/8, jumla ya shilingi milioni 617.1, zimetolewa kwa kaya 12,288 katika vijiji 88 vya halmashauri ya Arusha, huku kaya hizo zikipokea fedha kwa njia ya mitandao ya simu, benki, mawala na fedha tasmu.



# WANUFAIKA WA TASAF WAELEKEA KUFIKIA MALENGO YA MPANGO YA KUONDOA UMASIKINI

**Na Elinipa Lupembe**

Wananchi walio kwenye Mpango wa Kunusu Kaya Masikini kipindi cha pili awamu ya tatu, mradi unaotekelezwa na Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Halmashauri ya Arusha, wamekiri kuanza kuondokana na wimbi la umasikini uliokithiri, uliokuwa ukizikabili kaya zao na kuwa na mwelekeo wa kufikia malengo ya mpango huo.

Wanufaika hao wamekiri fedha hizo, kuwezesha kuondokana na wimbi la umasikini lililokuwa likizikabili kaya hizo, kwa kuanza kukuza kipato cha kaya na kuwezesha kaya kukua kiuchumi na kijamii huku watoto wakipata huduma za afya na elimu kwa amani na furaha, tofauti na hapo awali.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi kwa nyakati tofauti wakati wakupokea ruzuku ya dirisha la 6, wanufaika wa kijiji cha Oloigueruno kata ya Ilkiding'a, wamekiri fedha hizo za ruzuku kuwezesha kukuza kipato cha kaya kwa kuanzisha miradi na biashara ndogo ndogo.

Helena Lukumai (37), anayejishughulisha na bishara ya uuzaji wa viatu, amesema kuwa, pesa ya TASAF ndio imemuwezesha kupata mtaji wa kuuza viatu na tangu alipoanza kupokea pesa hizo alizikusanya mpaka kufikia shilingi elfu 80 na kupata mtaji wa kuanzisha biashara ya kuuza viatu.

Ameweka wazi kuwa awali hali ya maisha ya kaya yake haikuwa nzuri, hata kupata chakula cha familia ilikuwa ni changamoto, lakini kwa sasa ana uhakika wa famila yake kupata milo mitatu pamoja na kujikimu na mahitaji mengine ya nyumbani.

Naye Judith Paulo amebainisha kuwa, alianzisha mradi wa genge la kuuza mbogamboga, genge ambalo linafanya vizuri na kwa sasa kaya yake ina uhakika wa maisha, watoto wanapata chakula na mahitaji mengine kupitia genge hilo.

Neema Saitabau kijiji cha Lemanda, anyejishughulisha na biashara ya kuuza viazi soko la Oldonyosmabu, amesema kuwa, alikusnaya pesa za alizopokea TASAF na kupata elfu sitini na kuanza biashara ya kuza viazi kwenye magulio ya Oldonyosambu na Ngaramtoni.

"Nilianza na gunia moja kwa sasa nina mtaji wa magunia matatu, ninauza kwenye masoko ya Oldonyosambu na Ngaramtoni na ninategeme mtaji ukiongezeka kwenda kwenye masoko mengine zaidi". Amesisitiza Neema.

Hata hivyo wanufaika hao wameishukuru serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na mama Samia Suluhu, kwa kutoa elimu bila malipo mpaka kidato cha sita, jambo ambalo wamekiri kusaidia watoto wa kaya za walengwa wa TASAF, kuwa na uhakika wa masomo mpaka kidato cha sita kama ilivyo kwa watoto wengine.

"Zamani ilitulaizimu kutumia pesa hii ya TASAF kulipia watoto ada na michango mingine shuleni, baada ya serikali kuviondoa vyote, tumepata ahueni sana, pesa hizi zinatumika kufanya shughuli nyingine za kutuingizia kipato, kiukweli serikali imeturahisishia maisha kwa kiasi kikubwa mno".Amefafanua Anna Pendaeli

Naye Mratibu wa TASAF halmashauri ya Arusha, Grace Makema, amesema kuwa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi bilioni 2. 8 zimetumika kulipa walengwa hao kwa madirisha 6 huku jumla ya kaya 13,920 kutoka vijiji vyote 88 vya halmashauri hiyo zikinufaika na kuongeza kuwa, malipo yanayofanyika sasa ni dirisha la 6 na jumla ya shilingi milioni 568.8 zimegawiwa kwa kaya hizo.

Ikumbukwe kuwa lengo la Mpango wa kunusuru kaya Masikini kipindi cha pili cha awamu ya tatu mwaka 2020 mpaka 2023 ni kutoa fursa za kuongeza fursa za kujiongezea kipato na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii kwa kaya za walengwa pamoja na kulinda maslahi ya watoto kiafya na kielimu.



# WANUFAIKA TASAF ARUSHA DC WAFUNDWA

**Na Elinipa Lupembe**

Halmashauri ya Arusha inatekeleza mkakati wa kutoa elimu ya Ustawi wa Jamii kwa wanufaika wa mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, mradi unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo wanufaika hao wa matumizi ya ruzuku ya fedha wanazopokea ili kufikia malengo ya serikali.

Mratibu wa TASAF Halmasahuri ya Arusha, Grace Makema, amesema kuwa, kila zoezi la ugawaji fedha linapofanyika, watalamu huhakikisha wanatoa elimu kwa walengwa juu ya mambo muhimu ya kijamii, kwa lengo la kuwajengea uwezo wa namna bora ya matumizi ya fedha hizo, pamoja na kuwapa uelewa juu ya malengo ya serikali kutoa ruzuku hiyo kwa kaya zenye uhitaji.

Aidha amefafanua kuwa, serikali inatoa fedha hizo zikiwa na masharti ya kuzingatia, hivyo walengwa wa TASAF wanatakiwa kufahamu masharti ya fedha za ruzuku wanazopokea, pamoja na kuyatekeleza kwa usahihi, ikiwemo ruzuku ya msingi, ruzuku ya elimu na ruzuku ya afya kwa kaya hizo.

"Tunalazimika kutoa elimu, kutokana na uzoefu wa walengwa wanaopokea fedha kushindwa kutekeleza masharti na ruzuku na kusababisha kupoteza sifa, kama Halmashauri, tumejipanga kuwakumbusha kuzingatia masharti ya ruzuku ya fedha hizo, ikiwemo kuhakikisha watoto wanaosoma wanahudhuria masomo, watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kuhudhuria kliniki, na zaidi kuhakikisha ruzuku ya msingi inatumika kupata mahitaji muhimu na kuendelza pato la familia" ameweka wazi Mratibu Garace.

Naye Afisa Maendeleo ya Jamii, kata ya Mwandeti, Paulina Masoka, amekutwa na Kamera yetu akitoa elimu kwa Walengwa wa kijiji cha Losinoni kati, kata ya Oldonyowas, na kuweka wazi kuwa, ni kawaida kabla ya walengwa kupokea pesa, kupewa elimu ya masuala mbalimbali ya kijamii, yaliyopo na yanayoendelea kila siku.

"Hapa tunakumbushana, juu ya kuzingatia masharti ya ruzuku ya fedha wanazopokea pamoja na matumizi sahihi ya fedha hizo, zaidi tunawahamasisha kuunda vikundi vya kuweka na kukopa, lakini pia tumekumbushana juu ya malezi bora ya familia kwenye masuala ya Lishe bora na unyonyeshaji kwa watoto kwa siku 100, watoto kuhudhuria shuleni, kuwapeleka watoto kliniki, kujitokeza kuhesabiwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi mwezi Augost 2022, pamoja na kuwapeleka watoto kupata chanjo dhidi ya ugonjwa wa polio." ameweka wazi Paulina.

Hata hivyo wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya masikini, kijiji cha Losinoni kati, wamewapongeza wataalam kwa kuwapa elimu itakayowafanya kutambua msingi wa ruzuku ya fedha wanazopokea pamoja na malengo ya serikali ya kuzikwamua kaya hizo kutoka kwenye hali ya uamsikini.

Mwenyekiti wa kijiji cha Losinoni kati, mheshimiwa, Peter Gabriel, licha ya kuishukuru serikali kwa kutoa ruzuku kwa kaya zenye uhitaji, ameipongeza Halmashauri kwa kutoa elimu kwa walengwa wa TASAF, kutokana na ukweli kuwa elimu hiyo itawawezesha kujikwamua kijamii na kiuchumi, hali itakayosababisha kuondokana na wimbi la umasikini uliokuwa unazikabili kaya hizo.

Mnufaika wa TASAF, Amani Ngeresa amewashukuru na kuwpaongeza watalamu, kwa kuwapa elimu inayowezesha kutambua namna ya kuzingatia masharti ya ruzuku, matumizi sahihi ya fedha hizo, elimu iliyowawezesha kufahamu lengo la serikali la kuondoa umasikini kwenye kaya zao.

"Tunashukuru kwa elimu tuliyopewa, awali hatukufahamu kuwa pesa hizo zina masharti yake, na hatukufahamu lengo la Serikali kwa undani, lakini sasa tumejua serikali inataka nini kwetu, na tunaahidi kutumia pesa hizi, kuunda vikundi vya kuweka na kukopa ili kupata mitaji ya kuanzisha biashara ndogogo ambazo tunaamini zitatuondoa kwenye umaskini uliokuwepo." Amesisitiza mnufaika Amani.

Awali halmashauri ya Arusha, ni miongoni mwa halmashauri zinazonufaika na mradi wa Mpango wa Kunusuru kaya masikini, unaotekelezwa na TASAF III, huku jumla ya kaya 13, 859 katika vijiji vyote 88 vya halmashauri ya Arusha zikinufaika.

# WALENGWA WA TASAF WANAOJIMUDU KUONDOLEWA KWENYE MPANGO WA KAYA MASIKINI

Mtalamu ufuatiliaji kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF makao makuu, Judith Masika, amewasilisha utaratibu na maelekezo ya Serikali kupitia TASAF, wa kuanza mchakato maalumu kuwaondoa kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini, walengwa walioboreka kutokana na mpango huo na kukidhi vigezo vya kuweza kujitegemea, pamoja na kuanza malipo kupitia mfumo wa kielektroniki na kuondoa malipo ya fedha taslimu.

Mratibu huyo, amewalezea Waheshimiwa Madiwani wakati wa mkutano wa Baraza la Kata, uliofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa halmashauri ya Arusha kuwa, kutakuwa na zoezi maalum la kuwaondoa walengwa ambao wamekidhi vigezo kwa kuwa tayari wamekuwa na uwezo wa kuanzisha miradi inayowawezesha kujikimu kimaisha ili nafasi hizo zichukuliwe na walengwa wenye sifa ambao hawako kwenye mpango na wanakidhi vigezo vya kuingizwa kwenye mpango huo wa kunusuru kaya masikini.

"Zoezi hili litahusisha walengwa wa TASAF ambao tayari wameweza kujikimu kimaisha kwa kuanzisha miradi ambayo inawawezesha kupata mahitaji yao muhimu ya kimaisha na kukidhi vigezo vya kutokuwa kaya masikini tena, pamoja na baadhi ya walengwa kuingizwa kwenye mpango wakiwa hawana sifa, kwa kuwa wanauwezo na tunawafahamu kwa kuwa tunaishi nao katika maeneo yetu" Amesisitiza Judith

Aidha amelezea mabadiliko ya utaratibu wa serikali kupitia TASAF, wa kuwasajili walengwa kwenye mfumo ili waweze kulipwa ruzuku ya fedha kwa njia ya kielektroniki kupitia mitandao ya simu, benki na mawakala wa mitandao ya simu na kuachana na utaratibu uliopo wa kulipa fedha taslimu.

Amefafanua kuwa utaratibu wa kuwaondoa walengwa hao, utafanyika kupitia mkutano mkuu mkuu wa kijiji, na utahusisha walengwa wote walio kwenye mpango, kwa kuwasajili kwenye mfumo kupitia vitambulisho vyao vya Taifa (NIDA) na kusajili namba zao za simu na kwa walengwa wasio na simu wala akaunti za benki watatumia mawakala wa simu waliopo kwenye maeneo yao

Hata hivyo waheshimiwa madiwani walibainisha changamoto za maeneo yasiyo na mtandao ya simu, wazee wasio na simu na wale wasiojua kusoma na kuandika, wagonjwa na kaya ambazo zinaongozwa na watoto wasio na wazazi.

Mratibu huyo amefafanua kuwa, kwa walengwa ambao ni wazee sana, wasiojua kusoma na kuandika, wagonjwa, na kaya zinazoongozwa na watoto zitahudumiwa kupitia mawakala ambao wanasimamiwa na uongozi wa TASAF pamoja na program ya wasimamizi wa walengwa watakaochaguliwa kutoka kwenye jamii husika.

Aidha ameweka wazi faida za malipo kwa njia ya kielekroniki ni pamoja na usalama wa fedha za walengwa na kuondoa wizi na upotevu wa fedha, hali za udanganyifu, pamoja na kuwapa fursa walengwa kufanya maamuzi sahihi ya matumizi ya fedha, huku ikiokoa muda kwa walengwa badala ya kupanga foleni kusubiri fedha,watatumia muda huo kufanya shughuli nyingine za maendeleo za kuwaingizia kipato.

Awali, amewataka madiwani hao, kushirikiana na wananchi, uongozi wa vijiji katika maeneo yao, na kuwa mabalozi wazuri kwa kuweleimisha wananchi kutambua umuhimu wa zoezi hilo, lenye manufaa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.






# ARUSHA DC YAMSHUKURU MAMA SAMIA KUWAPATIA GARI LA TASAF

**Na Elinipa Lupembe**

Halmashauri ya Arusha, imepokea gari kutoka serikalini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF 'Toyota Land Cruser' lenye namba za usaji STM 0594, kwa ajili ya ufuatiliji wa utekelezaji wa miradi ya TASAF.

Mkurugenzi Mtendaji, halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, ameishukuru Serikali ya awamu ya sita, inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kwapatia gari kwa ajili ya kufuatilia miradi inyotekelezwa na TASAF katika halmashauri hiyo.

Mkurugenzi Msumi amemshukuru mheshimiwa Rais, kwa kuona umuhimu wa halmashauri kuwa na magari kwa ajalili ya miradi ya TASAF, huku akithibitisha kuwa gari hilo litarahisisha ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na TASAF katika vijiji 88, vya halmashauri ya Arusha, vinavotekeleza miradi hiyo ya TASAF.

"Kwa Jiografia ya halmashauri ya Arusha, kuna maeneo ambayo hayafikiki kirahisi kwa magari ya kawaida, ila uwepo wa gari hili utawarahisishia watalam kuifikia miradi na walengwa kwa urahisi na kwa wakati, jambo ambalo litawezesha halmashauri kufikia malengo yaliyokusudiwa na serikali, hususani kwenye miradi ya kaya zenye uhitaji zinazohudumiwa na TASAF". Amesistiza Mkurgenzi Msumi.

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF

HALMASHAURI YA ARUSHA
WILAYA YA ARUMERU

Imetolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Arusha


**Mhariri Mkuu:**
Seleman H. Msumi
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Arusha

**Mhariri Msaidizi:**
Elinipa J. Lupembe
Afisa Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Arusha

**Msanifu:**
Daniel Z. Gitaro
danielgitaro@gmail.com

Mawasiliano; S. L. P 2330, Arusha | Barua pepe : ded@arushadc.go.tz


Fuatilia kurasa zetu za Mitandao ya kijamii kwa habari na matukio mbalimbali zinazoenesha utekelezaji wa shughuli za Maendeleo katika Halmashauri ya Arusha kama zilivyoainishwa hapa chini.

www.arushadc.go.tz Arusha District Council arusha_district_council

enaboishu
FM RADIO 101.3